BISMILLAHIR RAHMANIR RAHIM.

Al hamisi tarehe23/Rabiul Thaany/1428 H =10/05/2007 M,
Pongwe-Tanga,Tanzania.makala namba 14.

# HII NDIYO DAAWA YETU

# JUU YA MAN'HAJI YA SALAF SWALIH.

MJUE MWANAWACHUONI MKUBWA SHEIKH MUHAMMAD AMAAN IBN ALLY AL JAAMY
KWA MTAZAMO WA MAULAMAA WALIOKUWA NA MSIMAMO WA KISALF KATIKA ZAMA HIZI NA UPOTOFU WA BARAHIYAN NA WASHIRIKA WAKE.

Aliulizwa Sheikh al Imam Abdul Aziz Ibn Baaz -Allah amrehemu-kuhusu Masheikh hawa wawili Rabii Ibn Haady na Sheikh Muhammad Amaan al Jaamy akasema;
"Ama kuhusu watukufu hawa wawili Sheikh Muhammad Amaan al Jaamy na Sheikh Rabii Ibn Haadi al Mad'khaly wote hao ni katika Ahli Sunna na ni maarufu kwetu sisi kuwa ni wenye elimu na fadhila na itikadi nzuri…
Kwa hiyo ninawausia kupata faida kutoka katika vitabu vyao…".
Athanaaul badi'I uk 13.

MUANDISHI;

ABUL FADHLI QASSIM MAFUTA QASSIM AL SALAFY.

بسم الله الرحمن الرحيم

Ewe mola wetu ni zako wewe sifa njema zote,na shukrani zote, ni zako wewe sifa njema vile zinavyo lingana na utukufu wako,na ukubwa wako,ni zako wewe sifa njema mpaka uridhike,na pale unaporidhika, na baada ya kuridhika.

Na sala na salamu zimfikie kipenzi chetu,Mtume wetu Muhammad, na jamaa zake,na maswahaba zake wote,na walioiandama njia yao kwa wema mpaka siku ya malipo.
Ama baada ya utangulizi.

Katika misingi mikubwa ya Ahli Sunna wal Jamaa ni kuwaheshimu maulamaa waliosimama kwenye haki na kuipigania na kuieneza katika maisha yao mpaka kufikia mwisho wa umri wao.

Na yoyote yule mwenye kuwatukana maulamaa wa Sunna bila ya hoja wala dalili kwa kuwabandika itikadi na misimamo potofu wasiyokuwa nayo atakuwa amefanya dhulma na hiyo ni ishara ya wazi ya kwamba mtu huyo hayuko katika njia ya sawasawa kama alivyosema al Imamu Abu Hatim;

وعلامة أهل البدع الوقيعة فى أهل الأثر !!!

“Alama za watu wa bid’a ni kuwatukana watu wa Sunna”!!!
Tazama Shar’hu usuli itikadi ah’li sunna cha imamu al Laalakai 1/179.

4- amesema Sheikh al Fawzani;

لا يقع على العلماء المستقيمين على الحق إلا أحد الثلاثة :
-إما منافق معلوم النفاق
وإما فاسق يبغض العلماء لأنهم يمنعونه من الفسق
وإما حزبي ضال يبغض العلماء لأنهم لا يوافقونه على حزبيته وأفكاره المنحرفة

“Hawatukani maulamaa walio katika mstari wa sawa,isipokuwa mmoja kati ya watu watatu;

-Ima atakua ni mnafiki anayejulikana kwa unafiki.
-ima atakua ni mtu muovu,anawachukia maulamaa kwasababu wanamkataza uovu wake.
-Ima atakua ni hiz’by (mtu wa vyama vya bid’a) aliyepotea, anawachukia maulamaa kwasababu hawaafikiani naye katika bid’a yake na fikra zake zilizopinda”.
Tazama al aj’wibatul mufida uk 75.

Na bila shaka vitendo vinavyofanywa na Salim Abdul Rahim Barahiyan na muajiriwa mwenzake Abu Hamza kutoka Mombasa Kenya vya kuwashutumu na kuwatukana maulamaa wa Sunna katika zama hizi kama vile;Sheikh Muq'bil Ibn Haadi al Waadi'i al Hamdaany -Allah amrehemu- na Sheikh Rabii Ibn Haadi Ibn Umayr al Mad'khaly -Allah amuhifadhi na kila shari- na Sheikh Muhammad Ibn Amaan Ibn Ally al Jaamy -Allah amrehemu- vitendo hivyo ni ishara ya wazi juu ya kupinda kwa fikra na misimamo yao na kuiwacha njia ya haki.

Na kusimama kuzitetea heshima za maulamaa hao na wengineo walio katika haki na kuwapa daraja zao ni jambo la wajibu kwa mwenye kuweza kulifanya hilo.
Na hilo ndiyo lengo la kuandikwa kwa makala hii.

## KWANINI TUNAMZUNGUMZIA SHEIKH AL JAAMY?

Nia na madhumuni yangu ilikuwa ni kuendelea na majibu ya kielimu dhidi ya mihadhara ya Salim Barahiyan ambayo imejaa uongo kejeli na propaganda.

Lakini baada ya kusikiliza maneno yake katika muhadhara uliofanyika katika msikiti wa Barabara sita Tanga mjini mnamo tarehe 02/05/2007 mhadhiri alikuwa ni Abu Hamza kutoka Chundwa (Lamu) na kutolewa utangulizi na Salim Abdul Rahim Barahiyan na maudhui ya muhadhara huo ulikuwa ni

السلفية وأدعياء السلفية

"Usalafi na wenye kudai usalafi".
Muhadhara ambao ulipoteza muelekeo wake na muhadhiri akashindwa kueleza kile alicho kusudia na ukisikiliza kwa makini muhadhara huo utagundua kwamba yule aliyeleta utangulizi (Barahiyan) ndiye aliye utawala muhadhara huo.

Na hakuna jambo lililonifanya niandike makala hii kwa haraka tena hata kufikia kuziacha makala nyingine ambazo zimekaribia kwisha bali nyingine zimekwisha ni kuitetea heshima ya Sheikh Muhammad al Jaamy ambayo imevunjwa kutokana na utovu wa adabu uliofanywa na Salim Barahiyan na aliyekuwa muajiriwa mwenzake katika taasisi ya al Muntada (Abu Hamza) dhidi ya mwanachuoni huyu ambaye ni miongoni mwa wanachuoni wa Sunna waliokuwa juu ya man'haji ya salaf swalih katika zama hizi.
Na bila shaka kufanya hivi ni wajibu kwa kila mwenye kuweza kufanya hivyo.

## HISTORIA FUPI YA SHEIKH MUHAMMAD AMAAN AL JAAMY.

Hii ifuatayo ni historia fupi ya sheikh huyu;

(a)Sheikh Muhammad Amaan Ibn Ally al Jaamy amezaliwa mwaka 1349H na kufariki mwaka 1416 H.

(b)Nafasi yake ya kielimu alikuwa na PHD katika mambo ya sheria ya kiislamu.

(c)Kazi zake za kidaawa, alikuwa ni mwalimu katika chuo kikuu cha Madina,na baada ya kustaafu kazi yake ya ualimu katika chuo kikuu hicho aliteuliwa kuwa mwalimu katika msikiti wa Bwana Mtume -rehema na amani zimfikie- Madina.

(d)Vitabu alivyoandika,Sheikh huyu ameandika vitabu vingi mno vilivyo na vilivyomashuhuri ni hivi vifuatavyo;

1-As sifaatul ilaahiyya fil kitabi wa Sunnatin nabawiyya.
2-Adh'waau alaa twariqi daawatil islami.
3-Manzilatus Sunnat fit tashriil islami.

## JE WANASEMA NINI MAULAMAA WA SUNNA KUHUSU SHEIKH HUYU?

Maulamaa wengi wa Sunna wamemsifia Sheikh huyu kwa kuwa na msimamo mzuri wa kisalafi katika uhai wake na baada ya kufa kwake,na hizi hapa ni baadhi ya kauli zao;

### 1)Amesema Sheikh Ibn Baaz Allah amrehemu;

"بخصوص صاحبي الفضيلة الشيخ محمد أمان الجامي والشيخ ربيع بن هادي المدخلي كلاهما من أهل السنة ومعروفان لدي بالعلم والفضل والعقيدة الصالحة ...فأوصي بالإستفادة من كتبهما...".
الثناء البديع ص13.

"Kuhusu watukufu wawili;Sheikh Muhammad Amaan al Jaamy na Sheikh Rabii Ibn Haady al Madkhaly wote hao ni katika Ah'li Sunna na ni maarufu kwangu kuwa ni wenye elimu na fadhila na itikadi nzuri… ninawausia kupata faida kutoka katika vitabu vyao..". uk 13.

وقال رحمه الله:
"وإخواننا المشايخ المعروفون فى المدينة ليس عندنا فيهم شك،هم أهل العقيدة الطيبة ومن أهل السنة والجماعة مثل الشيخ محمد أمان بن علي ومثل الشيخ ربيع بن هادي أو مثل صالح بن سعد السحيمي ....كلهم معروفون لدينا بالإستقامة والعلم والعقيدة الطيبة...".
الثناء البديع ص 13.

Na amesema tena;
"Na ndugu zetu masheikh ambao ni maarufu katika mji wa Madina hatuna shaka yoyote kwao, wao ni wenye itikadi nzuri na ni katika Ahli Sunna wal Jamaa mfano Sheikh Muhammad Amaan Ibn Ally na mfano Sheikh Rabii Ibn Haady au mfano Sheikh Swaleh Ibn Saad al Suhaimy…wote hao ni maarufu kwetu kwa msimamo na elimu na itikadi iliyo nzuri".!!!
Tazama kitabu al Qutbiyyah uk 183 na athanaaul badiu uk 13.

Huo ndiyo mtazamo wa Sheikh Ibn Baaz juu ya Mwanachuoni huyu aliyetukanwa na Salim Barahiyan na muajiriwa mwenzake wa al Muntadal Islami Abu Hamza.

Na ama baada ya kufariki sheikh huyu amesema sheikh Ibn Baaz;

"معروف لدي بالعلم والفضل وحسن العقيدة والنشاط فى الدعوة إلى الله سبحانه والتحذير من البدع والخرافات غفر الله له وأسكنه فسيح جناته وأصلح ذريته ...".

"Huyo ni maarufu kwangu kuwa ni mwenye elimu,fadhila na itikadi nzuri na nashati katika kulingania kwa Allah –Subhaanah- na kutahadharisha na bid'a na ukhurafi Allah amsamehe na amuweke katika nafasi pana ya pepo yake na amtangenezee kizazi chake…".
Cassette Haqiqatul Jaamiyyah ya Sheikh Abdul Aziz al Rayis.na tamko rasmi alilolitoa sheikh Ibn Baaz tarehe 9/Muharram/1418 H.

**2)Sheikh Swaleh Ibn Fawzaan al Fawzaan.**

Mnamo tarehe 5 Rabiul Thaany 1417 H Sheikh Swaleh al Fawzaan aliwataja maulamaa wa Sunna ambao wametoa juhudi kubwa katika kuineza daawa ya haki kwa kusema;

"كذلك من العلماء البارزين الذين لهم قدم فى الدعوة فضيلة الشيخ عبد المحسن العباد فضيلة الشيخ ربيع بن هادي كذلك الشيخ صالح السحيمي كذلك الشيخ محمد أمان الجامي إن هؤلاء لهم جهود فى الدعوة والإخلاص والرد على من يريدون الإنحراف بالدعوة عن مسارها الصحيح سواء عن قصد أو عن غير قصد هؤلاء لهم تجارب ولهم خبرة...

فيجب أن تروَّج أشرطتهم ودروسهم وأن ينتفع بها لأن فيها فائدة كبيرة للمسلمين". الثناء البديع ص 27.

"Vilevile miongoni mwa maulamaa waliodhihiri ambao wametangulia katika daawa ni Fadhilat Sheikh Abdul Muhsin al Abbaad na Fadhilat Sheikh Rabii Ibn Haadi na vilevile Sheikh Swalih al Suhaymi na vilevile Sheikh Muhammad Amaan al Jaamy.
Kwa hakika masheikh hawa wana juhudi katika daawa na ikhlasi na kuwajibu wale ambao wanataka kuipindisha daawa kutoka nje ya muelekeo wake wa sawasawa ni mamoja wanafanya hivyo kwa kukusudia au bila ya kukusudia,maulamaa hawa wana majaribio na uzoefu …kwahiyo inapasa kuzitawanya kanda zao na darasa zao na kunufaika nazo kwasababu mna ndani yake faida kubwa kwa waislamu". Athanaaul badiu uk 27.

وسئل الشيخ الفوزان فى الحرم المكي فى تاريخ 1424/6/13 هـ: هل من نصيحة لشباب يطعنون فى بعض أئمة الدعوة السلفية كالشيخ محمد أمان الجامي والشيخ ربيع الدخلي؟
فأجاب بقوله:" دعونا من الأفراد والقيل والقال والمشايخ إن شاء الله فيهم خير وفيهم بركة للدعوة السلفية وتعليم الناس فلو ما أرضو بعض الناس فالرسول ما أرضى كل الناس ...المشايخ نحسن بهم الظن وما علمنا عليهم إلا الخير إن شاء الله وندع لهم بالتوفيق".
الثناء البديع ص 28.

Na aliulizwa tena Sheikh al Fawzaan ndani ya msikiti mtukufu wa Makkah tarehe 13/6/1424 H;
Je kuna nasaha zozote kwa vijana ambao wanawatukana baadhi ya maimamu wa daawa ya Salaf kama vile Sheikh Muhammad Amaan al Jaamy na Sheikh Rabii al Madkhaly?
Sheikh akajibu;
"wacheni maneno ya baadhi ya watu na Qiila wa Qaala (porojo) masheikh hawa –Inshaallah- ni wenye kheri na baraka kwa daawa ya Salafi na kuwafundisha watu,ijapokuwa hawakuwaridhisha baadhi ya watu,na hata Mtume hakuwaridhisha watu wote…Masheikh hawa tunawadhania dhana njema na hatujui kwao ila kheri –Inshaalaah- na tunawaombea wao tawfiq". Kitabu hichohicho uk 28.

Aliulizwa Sheikh Swaleh Ibn Fawzaan al Fawzaan kuhusu maneno ya kash'fa juu ya vitabu vya Tawheed yaliyotolewa na bosi wa Salim Abdul Rahim Barahiyan na Abu Hamza (Muhammad Sururi Zainul Abidina anayeishi London Uingereza !!!!!) akasema sheikh Fawzaan;

"هذا القائل من دعاة الضلال نسأل الله العافية فيجب أن نحذر من كتابه هذا وأن نُحذِّر منه.

وأذكر لكم أن الشيخ محمد أمان الجامي – وفقه الله – قد أملى شريطاً كاملاً على هذه الكلمة ... ردًّا بليغاً فعليكم أن تبحثوا عن الشريط وأن تنشروه بين المسلمين حتى يحذروا من هذا الخبث ومن هذا الشر الوافد إلى بلاد المسلمين .
نعم هذا شريط قيم جدًّا جزى الله خيراً شيخنا الشيخ محمد أمان الجامي ونصر به الإسلام والمسلمين".
الأجوبة المفيدة عن أسئلة المناهج الجديدة ص 75 – 79.

"Huyu msemaji ni katika walinganizi wa upotevu –tunamuomba Allah atusamehe- ni wajibu kutahadhari na kitabu chake hiki(manhajul al anbiyaa) na kuwatahadharisha nacho watu.
Na ninakukumbusheni kwamba sheikh Muhammad Amaan al Jaamy – Allah ampe Tawfiq- amejaza kanda nzima juu ya kauli yake hii kwa majibu makali basi ni wajibu kwenu kuitafuta kanda hiyo na kuitawanya kwa waislamu ili watahadhari uchafu huu na shari hii inayoingia kutoka nje ya miji ya kiislamu!!.
Naam,kanda hii ni nzuri mno Allah amlipe kheri sheikh wetu sheikh Muhammad Amaan al Jaamy na Allah kwa (juhudi za sheikh huyu) aunusuru uislamu na waislamu".

Tazama kitabu al aj'wibatul mufidah uk 75-79.

Amesema Sheikh al Fawzaan baada ya kufariki Sheikh Muhammad Amaan al Jaamy;
"إن المتعلمين وحملة شهادات الشريعة كثيرون ولكن قليل منهم من يستفيد من علمه ويستفاد منه والشيخ محمد الجامي من تلك القلة النادرة من العلماء الذين سخَّروا علمهم وجهودهم فى نفع المسلمين وتوجيههم بالدعوة إلى الله على بصيرة من خلال تدريسه فى الجامعة الإسلامية والمسجد النبوي الشريف ....يدعو إلى التوحيد وينشر العقيدة الصحيحة ويوجه شباب الأمة إلى منهج السلف الصالح الخ ".
الشريط حقيقة الجاميةللشيخ عبد العزيز الريّس.

" Kwahakika wanaosoma na wenye kubeba shahada za sheria (ya dini) ni wengi mno,lakini ni wachache katika wao ambao wanafaidika na kupatikana faida kutoka kwao.
Na Sheikh Muhammad al Jaamy ni katika hao wachache walio nadra miongoni mwa maulamaa ambao wamezielekeza juhudi zao katika kuwanufaisha waislamu na kuwaongoza wao kwa kuwalingania kwa Allah kwa elimu kupitia kusomesha kwake chuo kikuu (cha Madina) na kusomesha katika msikiti wa Mtume mtukufu…..analingania Tawheed na kuieneza itikadi sahihi na anawaelekeza vijana kwenye Manhaji ya wema waliotangulia(Salaf Swalih)". Mpaka mwisho wa kunukulu.

Na aliulizwa Sheikh al Fawzaan alipokuwa akisherehesha Nuuniyya ya Ibnil Qayyim;

وسئل حفظه المولى فى شروحه على نونية ابن القيم:
يقول بعض الناس إن هناك فرقةً قد خرجت اسمها الجامية قد أطلقوها عليك فما أدري من أين أتوا بهذا الإسم ولماذا يطلقونه على بعض الناس؟
فأجاب حفظه الله تعالى:
"هذا من باب الحسد والبغضاء فيما بين بعض الناس ما فرقة جامية الشيخ محمد أمان الجامي رحمه الله تعالى نعرفه من أهل السنة والجماعة ويدعو إلي الله عزوجل ماء ببدعة ولا بشيئ جديد.
ولكن حملهم بغضهم لهذا الرجل أنهم وضعوا اسمه وقالوا فرقة جامية مثل ما قالوا الوهابية هذا عادة أهل الشر!!!!

ثم قال: "الحاصل إننا ما نعرف على هذا الرجل إلا الخير **والله ما عرفناه إلا الخير!**
ثم قال حفظه الله تعالى:
"...أنا أقول الآن هؤلاء عليهم أن يجيبوا (أن يأتوا) لنا الأخطاء التي أخطأ فيها هذا الرجل إذا جاؤوا بها ناقشناهاوقبلنا ما فيها من الحق ورددنا ما فيها من باطل أما مجرد الإتهمات والأقوال هذاما هو من شأن الحق اهـ.

"Wanasema baadhi ya watu kwamba kuna kundi limejitokeza jina lake ni Jaamiyya na pia wamekuita wewe (kuwa ni Jaamiya) sijui wamelitoa wapi neno hili na pia sijui kwanini wanawaita hivyo baadhi ya watu?
Akajibu Sheikh:
"Huo ni mlango wa hasadi na kuwachukia baadhi ya watu,hakuna kundi linaloitwa Jaamiya.
Sheikh Muhammad Amaan al Jaamy Allah amrehemu sisi tunamjua yeye ni katika Ahli Sunna wal Jamaa na analingania kwa Allah,na hakuja na bid'a wala jambo jipya.
Lakini ni chuki zao ndizo zilizowapelekea baadhi yao kumchukia mtu huyu na wakaliweka jina lake na wakasema kundi la Jaamiya kama walivyosema; hawa ni mawahabi!

Kisha akasema;"mwisho ni kwamba sisi hamtumjui mtu huyu ila kwa kheri.**Naapa kwa Allah hatumjui mtu huyu ila kwa kheri!!**

Kisha akaendelea kusema sheikh Fawzaan;

"Na mimi ninasema hivi sasa; hawa wanaodai hayo ni wajibu juu yao walete makosa ambayo amekosea mtu huyu wakiyaleta tutayajadili tutayakubali yale yaliyo na haki na tuyakataa yaliyo na batili.
Ama kutuhumu tu na maneno matupu si katika mambo ya haki".!!

Hebu tuyatafakari maneno ya mwanachuoni huyu(al Fawzaan) juu ya mwanachuoni mwenzake Muhammad al Jaamy;
Ukiwa ni mtu mwenye kutafakari utagundua yafuatayo;

a-Kuna vijana wanao watukana maulamaa hawa wakubwa wa kisalafi na bila shaka Salim Barahiyan na rafiki yake ni miongoni mwa vijana hao walio na utovu wa adabu dhidi ya maulamaa hawa.

b-Usia wa sheikh mwanachuoni mkubwa wa Sunna Sheikh al Fawzaan kwa waislamu ni kutosikiliza propaganda na porojo zao.

c-Sheikh Muhammad Amaan al Jaamy alimkosoa na kumjibu Boss wa al Muntada al Islami (Muhammad Suruar) taasisi amabyo makao yake makuu yako kule London Uingereza na Salim Barahiyan ni muajiriwa wa taasisi hiyo je unatarajia ndugu yangu muislamu kwamba Salim Barahiyan atakubali Boss wake akosolewe?

Kutanguliza mali mbele na kuitafuta dunia kwa jina la dini ni katika mambo mabaya yanayopelekea kuficha ukweli na haki katika dini.

d-Sheikh Muhammad Amaan al Jaamy ni katika masheikh wa kisalafi na wameiletea kheri nyingi daawa hii ya haki hata kama hawakuridhika maadui!

e)Sheikh Muhammad al Jaamy ni miongoni mwa maulamaa wachache ambao watu wamefaidika na elimu zao.

f)Alikuwa akilingania katika itikadi sahihi na kuwaongoza vijana kwenye manhaji (njia) sahihi ya wema waliotangulia (salaf swalih).

g)Namna hawa vijana walivyokuwa watovu wa adabu kwa maulamaa wamefikia kumuita sheikh al Fawzaan kuwa pia ni Jaamiya-kama wanavyodai-na hali ya kuwa hakuna kundi linaloitwa Jaamiya lakini chuki zao na hasadi ndizo zilizo wapelekea kutamka kauli hizi chafu dhidi ya mwanachuoni huyu.

h)Sheikh Fawzaan anaapa kwa jina la Allah kwamba hamjui Sheikh Muhammad alJaamy ila kwa kheri na wala hajaona shari kwake.
i)Lakini hii ndiyo ada na kawaida ya watu wa shari je Salim Barahiyan na rafiki yako mtalikwepa vipi kundi hili la watu wa shari wanao watukana maulamaa wa Sunna.

j)Hebu leteni makosa yaliyomtoa sheikh Muhammad al Jaamy nje ya daawa salafiya mpaka mkadai kwamba ndiye muanzilishi wa hiyo salafiya jadida mnayoidai.

Na kama msipoleta -na katu hamtoweza kufanya hivyo- basi mfahamu kwamba nyinyi ni watu waovu mliopinda katika fikra na itikadi hata kama mtalalamika.

Hawa maulamaa wa Sunna Ibn Baaz al Fawzaan wanamshudilia kwamba Sheikh Muhammad al Jaamy ni katika ahli Sunna wal Jamaa,Salafi anaye lingania watu katika njia ya salafi na hakuja na fikra mpya wala madhehebu mpya wala hakuasisi kundi jipya.

Wewe Barahiyan na rafiki yako mmezitoa wapi fat'wa hizi feki na uongo wenu huu wa kumzulia Mwanachuoni huyu mkubwa  au ni kwasababu tu amemkosoa boss?

Kuweni na adabu na maulamaa wa Sunna! Vipi mnawatetea maulamaa wa bid'a kwa hoja nyonge kabisa bali mpaka zindiki Ibn Sina mnamuadhimisha! bila ya hoja wala dalili na mkiambiwa oh! anataka kuvunja juhudi za taasisi!!! Je  mnataka dini nyinyi?

Lakini ameshasema Imamu Abu Hatim;

من علامة أهل البدع الوقيعة فى أهل الأثر !!

Miongoni mwa alama za watu wa bid'a ni kuwatukana watu wa Sunna!!

Na vilevile inatakikana mfahamu kwamba haifai kuwaadhimisha watu wa bid'a,
amesema Imamu Fudhail bin Iyadh;

(( من عظم صاحب بدعة فقد أعان على هدم الإسلام...))

شرح السنة للبربهاري ص **139**.

Mwenye kumuadhimisha mtu wa bid'a atakuwa amesaidia juu ya kuuvunja uislamu.
Shar'hu Sunna cha al Bar'bahary uk 139.

### 3-Sheikh Muhammad Abdul wahab al Banna;

قال الشيخ العلامة محمد بن عبدالوهاب البنا:
ولقد علمت بوفاة الشيخ محمد أمان الجامي – غفر الله له – وأسكنه فسيح جناته ولقد كان من المدافعين عن السنة والداعين إلى سلوك مذهب السلف أسأل الله أن يتقبل جهاده ويغفر لنا وله".

الثناء البديع ص 39. و مقدمة النصر العزيز للشيخ ربيع.

Amesema Sheikh Abdul wahab;

"Nimejua kifo cha Sheikh Muhammad Amaan al Jaamy –Allah amsamehe- na amuweke katika mahal pakunjufu katika pepo yake- alikuwa ni katika wenye kuitetea Sunna na ni mwenye kuilingania (kwenye Sunna) ".

**4-Sheikh Abdul Muhsin al Abbaadi;**

Amesema Sheikh Abdul Muhsin al Abbaadi kuhusu Sheikh Muhammad al Jaamy;

"...عرفته حسن العقيدة سليم الإتجاه وله عناية فى بيان العقيدة **على مذهب السلف** والتحذير من البدع وذلك فى درسه ومحاضراته وكتاباته غفرالله له ورحمه وأجزل له المثوبة اهـ.

"..Nimemjua yeye (Sheikh al Jaamy) kuwa ni mwenye itikadi iliyo nzuri na muelekeo uliosalimika na anatilia umuhimu sana **kubainisha itikadi juu ya msimamo wa Salaf** na kutahadharisha bid'a na anayafanya hayo katika darasa zake na mihadhara yake na vitabu vyake -Allah amsamehe na amrehemu na amlipe thawabu kwa wingi-".

**5-Sheikh Ally Ibn Hassan Ibn Abdul Hamid al Halaby mmoja katika wanafunzi wakubwa wa Sheikh al AlBany.**

Anasema Sheikh al Halaby;

"وهو الشيخ العلامة محمد أمان بن علي الجامي –تغمده الله برحمته-
وهو من المدرسين المشهورين –لسنوات كثيرة فى الجامعة الإسلامية فى المدينة النبوية.
وقد تخرج على يديه – فى العقيدة السلفية – مئات – إن لم يكن (ألوف) – من طلبة العلم والمشايخ والعلماء.
وتزكية سماحة أستاذنا العلامة الإمام الشيخ عبدالعزيز –يرحمه الله – له: مشهورة معلومة ...
ولا أعلم له يرحمه الله نهجاً خاصاً يسلكه فى الدعوة حتى يُنتَسبَ إليه ويجتمع عليه !!
والله تعالى يقول:( قل هاتوا برهانكم إن كنتم صادقين). والنبي يقول: (البينة على المدعي).

"Yeye ni Sheikh Mwanachuoni Muhammad Amaan Ibn Ally al Jaamy-Allah amfinike na rehma zake-
Na yeye ni katika waalimu waliomashuhuri-kwa miaka mingi katika chuo kikuu cha kiislamu Madina,wametoka kupitia yeye –kwa kuwasomesha itikadi ya Salaf- mamia –kama si maelfu- katika wanafunzi na masheikh.

Na Tazkiya ya Ustadhi wetu mwanachuoni Imam Sheikh Abdul Aziz –Allah amrehemu- kwa Sheikh huyu ni mashuhuri yenye kujulikana…

Na wala sijui kwamba-sheikh al Jaamy- Allah amrehemu- ana mfumo maalumu anaoufuata katika daawa mpaka ikafikia kumnasibisha nao au watu kujikusanya kwake!!
Allah anasema;

*"Leteni hoja zenu mkiwa nyinyi ni wakweli".*

Na Mtume anasema;

*"Kuleta ushahidi ni wajibu kwa mwenyekudai".mwisho wa kunukulu.*
Tazama http//www.alhalaby.com.

## NI WATU WA SAMPULI GANI WANAO MTUKANA SHEIKH MUHAMMAD AL JAAMY?

Hapo nyuma tumezitaja kauli nyingi za maulamaa wakubwa wa kisalafi kama vile;
Sheikh Abdul Aziz Ibn Baaz,Sheikh Swaleh Ibn Fawzaan al Fawzaan, Sheikh Abdul Wahab al Banna,Sheikh Abdul Muhsin al Abbaad al Badri, na Sheikh Ally Ibn Hassan Ibn Abdil Hamid al Halaby.

Maulamaa wote hao wamempa tazkiya kumtakasa Sheikh al Jaamy katika uhai wake na baada ya kufa kwake na baadhi ya maulamaa hao bado wako hai,hebu nendeni mkawaulize Sheikh Abdul Muhsin yuko hai Madina,Sheikh al Fawzaan yuko Riyadh Sheikh al Halaby yuko Jordan hebu waulizeni je kuna kundi linaloitwa Salafiya Jadida au Jaamiya lililoanzishwa na Sheikh Muhammad Amaan al Jaamy ?

Au na wao ni Masalafiya Jadida? hebu tuelezwe ukweli wala msibabaishe

Au ni uotovu wa adabu uliofanywa na waajiriwa na vibaraka wa al Muntada al Islami kuwatumikia mabwana zao walioko huko London?

Mbona hatukumsikia Naibu Mudir wa Ansaar Muslim Youth Centre akimkataza Boss wake kwamba usifanye hivyo maana ni wajibu wetu kuwaheshimu wanachuoni!
Maana Naibu Mudir wa AMYC alitoa muhadhara kamili na vilio juu, akinasihi watu wawaheshimu wanawachuoni.
Au mwanachuoni kwake yeye ni Boss wake Barahiyan tu? vilio vyote hivyo kumbe wamtetea Boss?!
Kupenda maslahi ya kidunia kutawapeleka watu mahali pabaya sana!

Boss wako kila uchao anawatukana maulamaa wa Sunna kwa jina la Sunna,amemtukana Sheikh Rabii,Sheikh Muq'bil,Sheikh Yahya alHajuur na mara ameanza kumtukana Sheikh Muhammad al Jaamy!

Na wewe uko hapo hapo kimya! Au hao wanaotukanwa kwako si maulamaa???
Huyu naibu mudir atakuwa na makala zake mbili maalumu –Inshaallah – ili kuwabainishia watu upumbavu aliouzungumza na huku akiangua vilio akijidai TAQIYYUN !!

Na nimeweka azma ya kumjibu kielimu kila atakayesimama kusema mambo bila ya elimu kwa ajili ya kutaka kuwababaisha watu juu ukweli wa daawa ya Salaf,hivyo basi mtu yoyote atakayejiingiza katika kundi la watu hawa atapata stahiki yake-Inshaallah-.

Sasa hebu tumsikilize Sheikh Abdul Aziz al Rayis anasema nini kuhusu wale wanaomtukana Mwanachuoni huyu je hao wanaomtukana ni maulamaa? Na je ni watu wa Sunna?
Ameanza Sheikh al Rayis kwa kuhoji kama ifuatavyo;

"لماذا ينبزون الدعوة السلفية باسم الجامية؟
"kwanini wanaibeza daawa ya Salaf kwa jina la Jaamiya?

"الجواب:لأن الدعوة السلفية تخالف دعواتهم وتخالف أحزابهم لما خالفت أحزابهم قاموا عليها قام عليها الإخوان المسلمون !!والقطبيون !! **والسروريون!!!** والتبليغيون والمتأثرون بهم سواء عن علم أو بغير علم مع ظني أن أكثر المتعاطفين مع هذه الجماعات هم فى الواقع غير عالمين بحقيقة هذه الجماعة وغير عالمين بحقيقة الدعوة السلفية..!!

Jawabu ni kwasababu daawa ya Salaf inatofautiana na daawa zao,pia na inatofautiana na vyama vyao kwahiyo ilipokuwa imetofautiana na wao walisimama kuishambulia,wamesimama Ikh'wanul Muslimun (Muslim Brotherhood) na Qutbiyyuun (wafuasi na walioathirika na Sayyid Qutbi kiitikadi na fikra) na Suruuriyuun (wafuasi na vibaraka wa Muhammad Surur Boss wa al Muntada al Islami kule London) na Matablighi na wale walioathirika nao ni mamoja wanafanya hivyo kwa elimu au bila ya elimu pamoja na kwamba katika dhana yangu ninadhania kwamba wengi wenye kujiunga na makundi haya kwahakika hasa si wasomi (wajinga) hawajui uhakika wa makundi haya na pia si wajuzi (wajinga)wa uhakika wa daawa ya Salaf..!!
Cassette Hakikatu al Jaamiya ya Sheikh al Rayis.

Kwa ufupi hao ndiyo wanaoitukana daawa ya Salaf na hao ndiyo wanaomtukana Sheikh Muhammad Amaan Ibn Ally al Jaamy –Allah amrehemu-.

Wote wameafikiana;

Ikhwanul muslimun na waathirika wao!!!

Wafuasi wa Sayyid Qutbi na wapenzi wake!!!

Suruuriyuun watu wa al Muntada al Islami na vibaraka wao!!!
Tablighi na mbegu zao!!!

Subhaanallah !!!! **تشابهت قلوبهم**
**"Nyoyo zao zimefanana"** wote hao wanamtukana! Kama alivyosema Imam Abu Hatim;

وعلامة أهل البدع الوقيعة فى أهل الأثر !!!

"Alama za watu wa bid'a ni kuwatukana watu wa Sunna"!!!
Tazama Shar'hu usuli itikadi ah'li sunna cha imamu al Laalakai 1/179.

Lakini masalaf na maulamaa wao kama vile Ibn Baaz,al Fawzaan,na al Abbaad wanamtetea na kuilinda heshima ya mwanachuoni huyu kwa kufuata ile kauli ya baadhi ya Salaf kama vile Imamu Qutaiba Ibn Said aliposema;

إذا رأيت الرجل يحب أهل الحديث فإنه على السنة ومن خالف هذا فاعلم أنه مبتدع !

" Utakapo muona mtu anawependa watu wa hadithi ( Sunna) basi huyo yuko katika Sunna na mweye kuhalifu hili basi ujue huyo ni mtu wa bid'a".
Tazama muqaddimatu shiari ah'lil hadithi uk 7.

Sasa hebu tuhoji kidogo;

Je Ibn Baaz kwenu nyinyi ni mtu wa Sunna Salaf au mtu wa bid'a hizbi?
Je anamtukana Sheikh al Jaamy kama nyinyi au anamtetea?
Kumbuka kwamba Ibn Baaz amesema kuhusu sheikh huyu;

"Huyo ni maarufu kwangu kuwa ni mwenye elimu,fadhila na itikadi nzuri…".!!

Je al Fawzaan naye?Je na yeye kwenu ni Salafiya Jadida?

Naye anamtukana Aalim huyu kama nyinyi na wenzenu matablighi na maikhwani? Au anaungana nasisi kwa kusema;

"Huo ni mlango wa hasadi na kuwachukia baadhi ya watu,hakuna kundi linaloitwa Jaamiya.

Sheikh Muhammad Amaan al Jaamy Allah amrehemu sisi tunamjua yeye ni katika Ahli Sunna wal Jamaa na analingania kwa Allah,na hakuja na bid'a wala jambo jipya..".rejea makala hii uk 8.

Nasisi tunasema hakuna kundi linaloitwa Jaamiya bali wale wote wenye kusema hivyo wamegubikwa na maradhi ya hasadi,chuki,ujinga na matamanio ya nafsi zao.

Na watutajie maulamaa watatu tu wa Sunna (na si wanaharakati mahizbi) waliomtoa mwanachuoni huyu nje ya njia sahihi ya Salaf Swalih na pia watutajie makosa yake ya kielimu ambayo yamemtoa nje ya njia sahihi ya wema waliotangulia (Salaf Swalih).

Ama kuhusu fat'wa yake ya kuhalalisha kuletwa majeshi ya Marekani nchini Saudi Arabia na Kuwait ili kutoa msaada wa kijeshi dhidi ya uvamizi wa Saadam Hussein hilo tunaliweka wazi katika sehemu hii ifuatayo;

## SHEIKH MUHAMMAD AL JAAMY NA FAT'WA YAKE YA KUHALALISHA MSAADA WA KIJESHI KUTOKA KWA MAKAFIRI.

Ulipotokea uvamizi wa Saadam Hussein dhidi ya nchi ya Kuwait maulamaa wa Saudi Arabia wote kwa kauli moja walitoa fat'wa juu ya uhalali wa kutaka msaada wa majeshi ya kikafiri (wamerikani).

Hakuna mwanachuoni yoyote ndani ya Saudi Arabia aliyejitokeza kwa uwazi kabisa kupinga fat'wa hii ya maulamaa hawa.

Bali ripoti iliyotolewa na mkutano wa maulamaa wa kiislamu kutoka sehemu tofauti za ulimwengu uliofanyika Makka al Mukarrama kuanzia tarehe 21 hadi 23/2/1411 H = 10 hadi 12 /09/ 1999 M.

Ripoti hiyo iliunga mkono fat'wa ya maulamaa hao ya kufaa kutaka msaada kutoka kwa makafiri kwasababu ya dharura za kisheria. Tazama ripoti hiyo katika kitabu Tawdhihul ahkaam cha Sheikh alBassaam alipokuwa akiisherehesha hadithi isemayo;
"ارجع فلن نستعين بمشرك" رواه مسلم من حديث عائشة رضي الله عنها.
"Rudi sisi hatutaki msaada wa mshirikina kabisa".

Pia kwa faida zaidi tazama maelezo ya Sheikh Ibn Uthaimin juu ya hadithi hii katika sherehe (maelezo) yake ya Bulughul maraami.

Kisha ufanye uwiyano na fat'wa iliyotolewa na Sheikh Muhammad al Jaamy je kuna tofauti yoyote? Au ni chuki na hasadi kwa Sheikh huyu kama anavyotueleza Sheikh Fawzaan?

Isipokuwa kuna baadhi ya vijana ambao wanaojiita wanaharakati walijaribu kuipinga fat'wa hiyo iliyotolewa na maulamaa wakubwa wakiongozwa na Sheikh al allaama Abdul Aziz Ibn Baaz.

Vijana hao waliipinga fat'wa hiyo kwa kejeli –kama kawaida yao- na kwa hoja nyonge mno! tena zinazoishiria uchochezi na machafuko ndani ya nchi hiyo.

Miongoni mwa walioshika bendera hiyo ya matusi dhidi ya maulamaa hao ni Muhammad Sururi Boss wa al Muntada!!

Hebu yasome maneno yake haya kwa makini halafu ujiulize je mtu wa Sunna anayehishimu fat'wa na rai za maulamaa wa Sunna katika mambo yaliyo na ikhtilafu anaweza kutamka maneno hayo?
Amesema Boss huyo wa al Muntada –hata kama wenyewe wanajaribu kumkana!-;
"وصنف آخر يأخذون –يعني: المساعدات الرسمية – ويربطون مواقفهم بمواقف ساداتهم...فإذا استعان السادة بالأمريكان انبرى العبيد إلى حشد الأدلة التي تجيز هذا العمل...وإذا انتهى الخلاف سكت العبيد...وهذا الصنف من الناس يكذبون ... ويتجسسون ...وإن أطالوا لحاهم وقصروا ثيابهم وزعموا أنهم حماة السنة ولا يضير الدعوة الإسلامية وجود هذا الصنف من الناس فالنفاق قديم...".

"Kuna kundi jingine ambalo linachukua misaada rasmi (ya serikali) na wanaifungamanisha misimamo yao na misimamo ya mabwana zao… Mabwana wakitaka msaada kutoka Marekani watumwa wanasimama kuzikusanya dalili ambazo zinahalalisha jambo hili…tofauti zikiisha watumwa nao wananyamaza…kundi hili linasema uongo…linafanya ujasusi …hata kama watarefusha ndevu zao na kupunguza nguo zao na wakadai kwamba wao ni watetezi wa Sunna lakini daawa ya kiislamu haidhuriki kwa kupatikana kundi hili la watu kwasababu **UNAFIKI NI WA KALE**…".

Tazama Gazeti lake analoliita "Sunnah" -Sheikh Muq'bil anasema Gazeti hili linastahiki kuitwa Gazeti la bid'a-! Gazeti hilo namba 23 la mfunguo tatu(Dhul Hijjah) mwaka 1412 uk 29-30.

Bila shaka ndugu msomaji anaposema kuhusu Saudi Arabia kwamba kuna maulamaa vibaraka watumwa wanachukua misaada rasmi ya serikali wanaandika ripoti wanafanya kila wanalolitaka mabwana zao!

Bila shaka atakuwa anawagusa moja kwa moja maulamaa waliopo katika jopo la maulamaa wa Saudi Arabia jopo ambalo linaongozwa na Sheikh Ibn Baaz! Pia akiwemo Sheikh Abdul Razaaq Afify,Fawzaan,al Sadlaan, al Ghudayyaan na wengineo je hawa ni watumwa na vibaraka?
Je hawa ni wanafiki???
Maana hawa ndiyo maulamaa wenye fat'wa rasmi zinazosikilizwa na serikali hiyo!

Basi kwanini Masheikh kama Muhammad al Jaamy,al Abbaad,Ahmad an Najmi,Swaleh as Suhaimy,Ubaid al Jaabiry na wengineo wasisimame kuwatetea maulamaa hawa ambao wamekuwa ni kinyang'anyiro cha mahizbi na wanaharakati tena kwa dhulma.

Naam kwa dhulma,maana wao ndiyo waliotoa fat'wa ya kuhalalisha kutaka msaada waislamu wa Bosnia kutoka kwa wakristo!!.

Na waliwahalalishia Wakurdi walioko kaskazini mwa Iraq kuchukua msaada kutoka katika nchi za magharibi.
Tazama madaarikin Nadhar uk 240 cha Sheikh Abdul Malik Ramadhan al Jazaairy.-Kitabu hicho kimepitiwa na Sheikh Al Bany na Sheikh Abdul Muhsin al Abbaadi na wamekisifia mno tazama utangulizi wao kwenye kitabu hicho-.

Na ndiyo haohao walio wahalalishia wanachama wa chama cha ISLAMIC SALVATION FRONT( FIS ) kilichopo nchini Algeria kutaka msaada kutoka Vatican!
Na hao (FIS) waliandika barua rasmi juu ya maombi yao hayo na barua hiyo ni ya tarehe 14/Rajab/1412 sawa na tarehe 19/1/1992.
Tazama kitabu hichohicho uk 257.

Sasa je ndugu muislamu huoni kwamba hawa watu walikuwa wamekusudia shari kwa kuwatukana maulamaa wa Sunna?

Ama maneno ya utovu wa adabu yaliyotolewa na Salim Barahiyan dhidi ya Aalim (mwanachuoni huyu) na hapa ninamnukulu kutoka katika kanda ya muhadhara uliofanyika tarehe 02/05/2007 katika msikiti wa Aali Sheikh barabara 6 Tanga.

Anasema Barahiyan –kwa ufedhuli-;

" Sasa hili,serikali ikaona (kwa maelezo ya muandishi wa kitabu hiki) Wizara ya mambo ya ndani ikaona kuna haja ya kupambana na masheikh hawa".

Akaendelea kusema;
"Sasa ninani mtu rahisi wa kuweza kumuuzia fikra hii? Ni sheikh huyu Jaamy.
Nayeye kwasababu alikuwa hakuwa na asili ya Usaudia alikuwa ni muhabeshi na ninii? Basi alikuwa ajipendekeze kwa upande wake aanze kutoa fat'wa juu ya uhalali".

Kisha akasema;
"Sasa huyu al Kannan –muandishi wa kitabu- anasema pakawa na makubaliano baina ya wizara ya mambo ya ndani na wafuasi wa Sheikh huyu,kwamba wizara ipate kuwaajiri watu waliosoma na baadhi ya masheikh iwe kazi yao sasa kutoa mihadhara ya kuwakandia hawa na ikiwezekana hatimaye watiwe ndani na kweli hilo lilifanyika".
mwisho wa kunukulu uongo wake.

Sisi jawabu yetu juu ya maneno haya ni kama ifuatavyo;

"Si kweli kwamba Sheikh al Jaamy alikuwa mtu rahisi wa kuweza kununuliwa kama wanavyonunuliwa wafuasi wa al Muntada ambao mgomvi wao ni yule anayemkosoa Boss wao!

Bali Sheikh al Jaamy alikuwa ni mwenye msimamo madhubuti kwenye njia ya sawasawa kwa ushuhuda wa maulamaa!!na inatosha kuwa maulamaa ni mashahidi kwasababu Allah mwenyewe amewafanya mashahidi.
Tazama Aala Imraan 18.

Ama kudai kwamba kulipita makubaliano baina yake na wizara ya mambo ya ndani ili kuwakandia baadhi ya masheikh,tunasema hizo ni porojo tu wala hazina dalili yoyote,na Bwana Mtume -rehma na amani zimuendee- amesema;

" كفى بالمرء إثما أن يحدث بكل ما سمع :

"Yatosha kwa mtu kupata dhambi kwa kujisemea kila analolisikia".
Ameisahihisha hadithi hii Sheikh al Bany tazama Sunan Abi Dawdi hadithi namba 4992.

Na kama mnao ushahidi basi mbona haukutajwa?
Makubaliano hayo yamefanyika wapi? Na lini?

Ni kina nani waliohudhuria makubaliano hayo? Hebu tutajieni!

Na vipi Sheikh akubali kufanya makubaliano amabyo si ya haki-kama mnavyodai- kisha maulamaa wenzake –kv Ibn Baaz,Fawzaan,al Abbaad na wengineo wasiseme chochote bali wamsifie kwa sifa kemkem ?!

Hivi kweli inatosha mtu kuamua kumtuhumu mwenzake bila ya ushahidi wowote halafu watu waufanyie kazi?

Mbona wewe ulipotuhumiwa kwamba ni Shushu (……)!!!
Ulilalamika na kudai unaonewa na ukalazimisha upewe ushahidi?

Je hili la kutaka ushahidi halina nafasi kwa watu wengine? Insafu na uadilifu uko wapi?

Mbona ulipotuhumiwa wewe kwamba ni kada wa chama fulani cha siasa ulihamaki na ukadai ushahidi na ukawatuhumu hao wanao kutuhumu kuwa ni maadui wa Taasisi yako?

Je haya hayastahiki kufanyiwa watu wengine? Tena maulamaa wa Sunna?

Ama kuhusu kufungwa na kuzuiliwa kutoa mihadhara na darasa kwa masheikh hao wanaoitwa masheikh vijana kama vile;

Salmaan Ibn Fahd al Awdah na Safar Ibn Abdil Rahmaan al Hawaaly ukweli ni kwamba masheikh hawa walikuwa wakilingania kwenye batili jambo ambalo limepelekea Daarul Iftaai (majlis ya fat'wa) ya Saudi Arabia ikiongozwa Sheikh Abdul Aziz Ibn Baaz walipitisha mswada wa kuzuiliwa watu hawa kufanya daawa ili kuzuia upotofu wao huo usije ukaenea,kisha wakaupeleka mswaada huo Wizara ya mambo ya ndani ya Saudi Arabia ili kulitekeleza agizo hilo la maulamaa na mwisho wa makala hii tunambatanisha copy ya barua hiyo ambayo ina muhuri wa pete ya Sheikh Ibn Baaz ili ujionee mwenyewe!

Swali je maulamaa hao wa Daarul Iftaai nao walinunuliwa na Wizara kwa kujipendekeza? Mbona tuhuma hizo zinapelekwa kwa Sheikh Muhammad al Jaamy pekeyake?
Ni nini kama si hasadi na chuki binafsi?!kama anavyosema sheikh Fawzaan.

ERROR: undefined
OFFENDING COMMAND: low

STACK:

-mark-
/shaddah